

Kuzuia Viwavijeshi kwenye mahindi

Spodoptera frugiperda



KUZUIA

- Panda mimea mapema wakati wa mvua za kwanza kwa sababu Viwavijeshi (FAW) huongezeka baadaye katika msimu wa mimea.
- Epuka kupanda nyakati tofauti tofauti kwa kuwa kufanya hivi huwapa Viwavijeshi chakula muda wote.
- Panda aina za mbegu za mahindi ambazo zinastahimili Viwavijeshi ikiwa zinapatikana.
- Tumia mitego ya kuwanasa nondo ili kubaini mapema uwepo wa kiwavijeshi vamizi
- Panda mbegu za mahindi zinazokomaa baada ya muda mfupi.
- Hakikisha unatumia mbolea kikamilifu ili upate mahindi bora ambayo yanaweza kustahimili uharibifu unaotokana na wadudu.
- Kilimo mzunguko kwa kubadilisha mazao jamii moja na nyingine
- Ondoa magugu katika eneo linalozunguka shamba.
- Panda ua za miti ya jami kunde au ya maua ya mwaka mzima yakiizunguka bustani, inavyowezekana, ili ujenge makazi ya wadudu wenye manufaa, ndege na wanyama wala wanyama.
- Panda mahindi pamoja na mimea mingine isiyoharibiwa kwa urahisi na wadudu kama vile maharage na mihogo.

